JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

"Kilimani" Iringa Road,
S.L.P. 1175,
41101 DODOMA,
Barua Pepe: rbcdodoma@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

DODOMA – OKTOBA 24, 2020

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

WANANCHI WANYONGE WAREJESHEWA FEDHA ZAO

Lengo la kuanzishwa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na rushwa (TAKUKURU) ni kuondoa rushwa na kuimarisha utawala bora. Palipo na dhuluma hakuna utawala bora, hivyo tunapenda kuutaarifu umma juu ya juhudi za Serikali katika kutetea haki na hivyo kuimarisha utawala bora, ambapo leo tumewezesha kurejesha kwa wananchi wawili wanyonge jumla ya shilingi milioni ishirini na nane mia tisa sabini na tano elfu mia tano sabini na nane (28,975,578/=).

Kwanza, tunamrejeshea Mwalimu Mstaafu **Bw. Stanley Godfrey Matonya,** Mkulima wa Kijiji cha Itiso wilaya ya Chamwino, kiasi cha shilingi 22,485,000/= alizodhulumiwa na Kampuni ya Kabugama (Kabugama Co. LTD) ya Jijini Dodoma tangu mwaka 2016. Agosti 2016, Mstaafu huyo aliingia mkataba wa kuuziwa trekta na Kampuni hiyo na Oktoba, 2016 alipaswa kupatiwa trekta moja aina ya Swarrag 744 lenye jembe moja pamoja na tela kwa maelewano ya kulipa shilingi 23,985,000/= ambayo ni asilimia hamsini ya thamani ya trekta. Pamoja na kulipa kiasi hicho tangu Septemba, 2016 kulingana na mkataba, mwananchi huyo hakupatiwa trekta na alipofuatilia aliambulia kurejeshewa shilingi 1,500,000/= tu. Baada ya kuona juhudi zake zote za kulipwa zimekwama, Agosti mwaka huu, alitoa taarifa TAKUKURU na uchunguzi wetu umewezesha kampuni hiyo kurejesha kiasi cha shilingi 22,485,000/= ambazo Bw. Matonya anakabidhiwa leo.

Pili, pia tunamrejeshea **Bw. Ahmed Talibu,** mkazi wa Jijini Dodoma ambaye ni mzazi wa mtoto Nasra Ahmed Talibu kiasi cha shilingi milioni sita mia nne tisini elfu mia tano sabini na nane (6,490,578/=) zikiwa ni malipo ya fidia ya kiwanja namba 214 Kitalu G Kikuyu South Extension Jijini Dodoma kilichotwaliwa kwa ajili ya kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya mwendokasi. Mei mwaka huu TAKUKURU Mkoa wa Dodoma ilipokea taarifa kutoka kwa Bw. Talibu kwamba ameshindwa kulipwa baada ya kuelezwa na Shirika la Reli linaloratibu zoezi hilo kwamba tayari malipo hayo ya fidia ya kiwanja cha mwanaye yalishafanywa kwa mwananchi mwingine.

Uchunguzi wetu ulibaini kuwa malipo ya fidia ya kiwanja hicho yalifanywa kwa **Bi. Noorjan Abdulhamid Ahmed** baada ya kuwasilisha nyaraka alizozipata alipouziwa eneo hilo kwa njia ya udanganyifu. Ufuatiliaji zaidi wa TAKUKURU ukawezesha Bi. Ahmed ambaye hakuwa mmiliki halali wa kiwanja hicho kurejesha fedha alizolipwa bila kustahili ambazo leo tunampatia Bw. Talibu kwa niaba ya mtoto wake. Aidha, juhudi zinaendelea kumtafuta Mtuhumiwa aliyemwuzia kwa njia za hila na kumpatia Bi. Ahmed nyaraka za kiwanja hicho ili hatua stahiki zichukuliwe dhidi yake.

Tatu, Tunawafahamisha pia kwamba Mahakama mkoani Dodoma zimetoa maamuzi ya mashauri manne na kuwatia hatiani washtakiwa watano kwa makosa mbalimbali ya rushwa.

- Uamuzi wa shauri la jinai namba 148/2019 ulitolewa tarehe 19/10/2020 ambapo Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma imewahukumu wafanyabiasha wa Jijini Dodoma **Bw. Nahid Bahadur Hirji** na mwanaye **Bw. Bahadur Abdallah Hirji** kulipa faini ya jumla ya shilingi 1,500,000/= au kwenda jela miaka mitatu baada ya kukiri mashtaka matatu ya kuahidi na kutoa rushwa ya shilingi 1,200,000/= kwa aliyekuwa Mkuu wa wilaya ya Dodoma **Bw. Petrobas Katambi** kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007. Julai, 2019 TAKUKURU iliwafikisha wafanyabiashara hao mahakamani baada ya uchunguzi kuonyesha kwamba walifanya jinai hiyo kama kishawishi ili hatua stahiki zisichukuliwe dhidi yao kuhusiana na

mgogoro wao wa kifamilia. Aidha, Mahakama imetaifisha shilingi 1,200,000/= zilizokamatwa wakati wa mtego wa hongo.

- Mahakama ya wilaya ya Kongwa imetoa uamuzi wa shauri la uhujumu uchumi namba 1/2019 na imemhukumu Bi. **Mary Baltazary Lema** aliyekuwa Mwalimu wa shule ya Msingi Miembeni wilayani Kongwa kulipa faini ya shilingi 300,000/= au kwenda jela mwaka mmoja, na kuirudishia Serikali kiasi cha shilingi 5,459,628/= alizohusika kuisababishia hasara kinyume na Sheria ya Uhujumu Uchumi.

  Mahakama hiyo pia imetoa uamuzi wa shauri la jinai namba 122/2020 na kumhukumu **Bw. Aidan Ainea Mganga** ambaye ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Makawa-Kongwa kulipa faini ya shilingi 500,000/= au kwenda jela miaka mitatu baada ya kukiri shtaka la kupokea rushwa kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.
- Aidha Mahakama ya Wilaya ya Kondoa imetoa uamuzi wa Shauri la jinai Na. 60/2020 na kumhukumu **Bw. Abasi Shabani Saidi** ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa wa Tampori wilayani Kondoa kulipa faini ya jumla ya shilingi 600,000/= au kwenda jela mwaka mmoja baada ya kukiri mashtaka mawili ya kushawishi na kupokea rushwa ya shilingi 120,000/= kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Mwisho, TAKUKURU Mkoa wa Dodoma inawakumbusha wananchi kwamba Serikali haivumilii vitendo vya dhuluma kwa wananchi wake kwani ni kinyume na misingi ya utawala bora, hivyo ni wajibu wa kila mwananchi kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za utendaji na utoaji huduma. Tukumbuke, uchaguzi ulio mbele yetu ni fursa ya kuimarisha utawala bora kwa kushiriki na kuchagua viongozi wanaojali wananchi wanyonge na wanaoichukia rushwa.

Imetolewa na:

Sosthenes Kibwengo
Mkuu wa TAKUKURU (M) Dodoma